

*Hili ni jibu la Alhaj Sheikh Yusuf Kalala kwa shairi lililotungwa na LGFumbuka kufuatia mjadala kuhusu sera za Rais Benjamin Mkapa.*

**WAPI MBELE KAKOSEA, KOSA LAKE KOSA GANI?**

- |  |  |
|--|--|
| <p>01. Fumbuka umenitoa, huku nilikojifichia<br/>Barua uliyomuandikia, Azizi kaipokea<br/>Hapo chini najionea, macho yamekodolea<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>02. Sikutaka kuingia, haikuwa yangu nia<br/>Mjadala kuuchangia, kweli sikutarajia<br/>Ila ulipowania, U-spin doctor kunigea<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>03. Leo nitakuvamia, kamwe sitakuachia<br/>Mwenyewe umejitakia, huna wa kukulilia<br/>Huna wa kukuamua, wala atayekukwamua<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>04. Fahari wajipachikia, huna wa kukusifia<br/>Makofi wanaokupigia, ndio wataokuzomea<br/>Hoi watakuachia, hapo utapohitimia<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>05. Nafasi takutafutia, muda utaohitajia<br/>Uweze kuelezea, hoja kutupangia<br/>Kosa alotufanyia, huyu Mbele maridhia<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>06. Fumbuka kwanza tulia, uweze kuzingatia<br/>Huko ulikoanzia, mjadala kutokezea<br/>Bila kufuatilia, vigumu kuashiria<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>07. Bure wampakazia, tena unamuonea<br/>Huruma imekuishia, heshima kumpunguzia<br/>Meya ana waenzimia, wengi wana mstahikia<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>08. Kusoma nimerudia, yote alotuandikia<br/>Kosa sikujionea, ila kuzidi mkubalia<br/>Naona wamsingizia, na kejeli kujazia<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> | <p>09. Mbele kautangazia, Tanzaneti na umatia<br/>Kisha katulingania, tuungane kugombea<br/>Heshima inayopotea, ya Taifa na jamia<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>10. Wazi kaelezea, si kihamba Tanzania<br/>CCM kuchezea, hilo kajikatalia<br/>Na serikali sawia, nalo kaligomea<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>11. Mbele katuorodheshea, kero zilizotangulia<br/>Shingoni zimetukalia, hatuna pakuhemea<br/>Bayana katuwekea, ukumbini kahadithia<br/>Wapi mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>12. Mwembechai katutajia, na Kilombero pia<br/>Unguja hakumezea, Pemba hakuachilia<br/>Kipi kabakizia, ambacho hakikutokea?<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>13. Ni kipi kaongezea, Fumbuka ulichokichukia<br/>Au hutaki kusikia, ukweli kubainishia<br/>Si vizuri kuzingua, watu watakukimbia<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>14. Wakimbizi kukimbia, Mombasa kuelekea<br/>Majini kufarikia, na majeraha kuzagaa<br/>Misikitini kuulia, magerezani kutesea<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>15. Maandamano kuzuia, hiyo ni yenu tabia<br/>Vurugu kuwaanzia, askari kuwapelekea<br/>Virungu kuwapigia, mkong'oto kutembezea<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> <p>16. Uchaguzi kubomoa, wakati ulipo wadia<br/>Masanduku kujifichia, kura nyingi kupotea<br/>Wala hatukujua, pale mlipohesabia<br/>Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?</p> |
|--|--|

17. Ushindi kujitangazia, hayo tumeyazoea  
Kishindo kujiongezea, lipi la kushangazia  
Yote tunayajua, tumeshindwa kuvumilia  
Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?
18. CCM umezidia, mno kuisifia  
Na serikali pia, sana waipendelea  
Umeshindwa kuwakosoa, wanapotuchemshia  
Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?
19. CCM kuikwamua, Fumbuka umepania  
Tena umedhamiria, mizengwe kutupangia  
Uchafuwe kuufukia, hilo unaliwania  
Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?
20. Himiza kuelezea, Mbele alofanyizia  
Kosa tupate tambua, mbele kutuwekea  
Wazi kutufunulia, yapate kutuelea  
Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?
21. Mbele katuusia, vibaya kunyamazia  
Tukishindwa kuchukua, zinazofaa hatua  
Basi bora kulia, kelele kujipigia  
Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?
22. Kama Mkapa kaamua, Upinzani kuusikia  
Kibao kakuguezia, sote tunashangilia  
Serikali tumeridhia, yetu sote twafurahia  
Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?
23. Nchi aliiachia, akatutilia ghasia  
Soni akayaonea, majeshi ya Tanzania  
Akaacha kukemea, sasa amegundua  
Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?
24. Mengi nimeyafungia, mwangu katika kifua  
Bora nikabakizia, moyoni kuyabanishia  
Huenda nikayatoa Itakapo nilazimia  
Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?
25. Fumbuka nakungojea, na wanao shangilia  
Kamwe sitaridhia, Mstahiki kuangukia  
Hapa nimepoa, majibu nasubiria  
Wapi Mbele kakosea, kosa lake kosa gani?

*Yusuf M. Kalala,  
Washington DC., USA  
02-02-02*